www.xtrapapers.com

N15/2/ABSWA/HP1/SWA/TZ0/XX/T

Diploma Programme
Programme du diplôme
Programa del Diploma

# Swahili B – Higher level – Paper 1
# Swahili B – Niveau supérieur – Épreuve 1
# Swahili B – Nivel superior – Prueba 1

Monday 9 November 2015 (afternoon)
Lundi 9 novembre 2015 (après-midi)
Lunes 9 de noviembre de 2015 (tarde)

1 h 30 m

---

**Text booklet – Instructions to candidates**

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for paper 1.
- Answer the questions in the question and answer booklet provided.

**Livret de textes – Instructions destinées aux candidats**

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

**Cuaderno de textos – Instrucciones para los alumnos**

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

8 pages/páginas

8815 – 2316
© International Baccalaureate Organization 2015

International Baccalaureate
Baccalauréat International
Bachillerato Internacional

www.xtrapapers.com



Blank page
Page vierge
Página en blanco

www.xtrapapers.com



**Kifungu A**


# Nyama ya Mbuzi ya Kukaanga

❶ Nyama ya mbuzi ni moja kati ya vile vyakula ambavyo watu wengi au familia nyingi za pwani ya Kenya hula hasa wakati wa sherehe kama vile harusi kwa hamu sana. Kwa sababu mbuzi hula majani tofauti, hudhaniwa hutibu magonjwa tele. Ni moja kati ya vile vyakula ambavyo watu hupania kula. Sasa hivi imekuwa ni dhana kuwa nyama ya mbuzi ni lazima ichomwe na wengi wamezoea kwamba nyama hii huliwa kwa baa. Mara nyingi ukisikia watu wanaongelea juu ya kula nyama ya mbuzi, utasikia jina la baa au mahali fulani pa nyama choma pakitajwa. Mara nyingi watoto wamekosa kula nyama ya mbuzi kwa sababu mama na baba zao huila kwa baa.

❷ Nyama ya mbuzi kama ilivyo ya ng'ombe au kuku huweza kuandaliwa na kupikwa nyumbani kwa ajili ya mlo wa familia. Kuna namna nyingi sana za kuandaa na kupika nyama ya mbuzi na mojawapo ni kukaanga kwa mafuta machache. Namna hii ya upishi wa nyama ya mbuzi ingawa ni rahisi na ya haraka, ina ladha nzuri na ni rahisi kula hata kwa watoto ukilinganisha na nyama ya kuchoma.

**Mahitaji**

❸
- Nyama ya mbuzi kilo moja.
- Chumvi kwa ladha uipendayo.
- Vitunguu saumu iliyopondwa/sagwa kijiko kimoja na nusu cha chai.
- Tangawizi vijiko vitatu vya chakula.
- Mafuta ya kupikia nusu kikombe.
- Vijiko vitatu vya chakula vya limau.



**Njia**

❹ Baada ya kukata na kuosha nyama ya mbuzi, toa maji yote kwenye nyama kisha weka kwenye sufuria utakayopikia. Ongeza chumvi, limau, vitunguu saumu na maji ya tangawizi katika nyama, kisha changanya vizuri ili viungo visambae kwenye nyama.
Weka jikoni na uchemshe huku ukiwa umefunika. Usiweke maji kwenye nyama kwani nyama huwa na maji mengi ya asili. Pale tu nyama inapoanza kuchemka, igeuze na uendelee kuigeuza kila baada ya dakika mbili ili iive yote kwa pamoja na pia ili viungo viendelee kusambaa.

❺ **Maelezo ya ziada**

Usiweke viungo vingi kwani vitapoteza ile ladha ya mbuzi. Lengo la kuweka vitunguu saumu, maji ya tangawizi na limau ni kuondoa harufu ya mbuzi na pili ni kuboresha ladha ya nyama.

❻ Zingatia utumiaji wa maji au mchuzi wa tangawizi, usiweke tangawizi iliyopondwa au kusagwa na wala usitumie tangawizi ya unga. Lengo hapa ni kuepuka kutafuna kiungo unapokula. Viungo vyote vinatakiwa kupotelea ndani ya nyama. Mpaka hapo, nyama ya mbuzi ya kukaanga iko tayari na inaweza kusindikizwa na chakula chochote. Mimi napenda zaidi kusindikiza na ugali na mboga ya majani.

Imetoholewa kutoka, www.tollyzkitchen.wordpress.com (2013)

www.xtrapapers.com



**Kifungu B**

## Maajabu Ya Dunia: Nyumbu Wathibitisha "Nyumbani" Kwao Ni Serengeti

❶ Maelfu ya maelefu ya makundi ya wanyama aina ya nyumbu, wanaokadiriwa kufika zaidi ya milioni 1.5 wameanza kurejea nyumbani katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti wakitokea mbuga ya wanyama ya Masai Mara nchini Kenya walikoenda kwa mapumziko ya muda mfupi.

❷ Tukio la kurejea nyumbani kwa nyumbu hao huwavutia watalii wengi mno kutoka sehemu mbalimbali duniani kuja kujionea kwa macho yao wenyewe badala ya kuangalia kwenye runinga.

❸ "Sina maneno ya kuelezea furaha yangu kuhusu hiki nilichokiona moja kwa moja kwa macho yangu… nimepata tu kuona makundi ya nyumbu hawa wakivuka mto huu kupitia kwa mkanda wa picha uliorekodiwa, lakini sasa imekuwa ni maajabu kweli kushuhudia hali hii", anasema mtalii mmoja kutoka Uholanzi akiwa na mumewe. Yeye na mumewe wakiwa ni miongoni tu mwa watalii wengi wanaotembelea Serengeti kujionea maajabu hayo, anasema amekaa kwenye mbuga hiyo kwa siku ya tano akisubiri kuona jinsi makundi ya nyumbu yanavyovuka mto huo kwa pamoja.

❹ "Nafikiri nimekuwa mwanamke mwenye bahati sana kushuhudia uhamaji wa makundi ya nyumbu yakivuka mto […] hakika sina maneno zaidi ila haya ni maajabu ya dunia". Anasema Serengeti ni mbuga nzuri yenye kuvutia ndiyo maana inatambuliwa kama ni moja ya Maajabu Saba ya Dunia.

❺ Anasema walianza safari yao katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ambayo imejaa wanyama wengi wakiwemo tembo na walitaka kufurahisha nyoyo zao kwa kushuhudia makundi ya nyumbu yakihama na jinsi yanavyovuka mto huo.

❻ Mto Mara umeanzia Kenya na kupita katika hifadhi ya Serengeti hadi ziwa Victoria ambako humwaga maji yake. Ili kutunza mto huo ambao ni muhimu kwa maisha ya wanyama, mradi wa kuutunza umeanzishwa kwa ushirikiano wa nchi mbili hizi, mradi ambao huangalia maeneo mbalimbali ya mto huo ili mazingira yake yasiharibiwe.

❼ Wawapo Serengeti, watalii wengi wanapenda kuangalia makundi ya wanyama hao wanapochukua muda mrefu kujishauri namna ya kuvuka mto Mara, wenye viboko wengi lakini hofu kubwa inayowakumba nyumbu ni mamba ambao wamekuwa hatari kwao.

❽ Ukiwasikiliza wanyama hao, sauti yao hutoa burudani ya aina yake ambayo utapenda kuendelea kusikiliza. Wakati fulani nyumbu watoto huanza kujaribu kuvuka na kufuatiwa na wakubwa lakini wagusapo maji na kuhisi kwamba kuna mamba, basi kundi zima hurudi nyuma kwa kukimbia ovyo.

❾ Baada ya kurudi nyuma, huwachukua tena muda mrefu na wakati mwingine hukimbilia eneo lingine mbali kujaribu kuvuka na kufanikiwa kufanya hivyo kwa hata baada ya saa zaidi ya tano. Meneja wa Uhusiano wa Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA), anasema watalii wengi wamekuwa wakipanga safari za kutembelea hifadhi hiyo ikiwa ni pamoja na kujionea makundi ya wanyama wakiwa wanarejea nyumbani na namna wanavyovuka mto. Wanyama hao hufanya hivyo wakati wowote kuanzia macheo hadi magharibi wanapoacha shughuli hiyo. Asema mto Mara ni kizuizi kikuu kwa wanyama na wafikapo ukingoni, huchukua muda mwingi kuvuka.

John Ngunge, *Nipashe* (2012)

www.xtrapapers.com



**Kifungu C**

# Hongera Kampuni Mashuhuri Kufadhili Mashindano Ya Ngoma Za Kisukuma



Kundi la ngoma la Makilikili kutoka Shinyanga

❶ Kwa muda sasa nimekuwa nikiyashutumu makampuni mbalimbali hapa nchini kwa kuwa maajenti wa utandawazi. Kwa mfano, nimekuwa nikijiuliza: ni kwa nini makampuni haya yamejikita zaidi katika kudhamini mashindano ya urembo ambayo yamezagaa katika kila kona ya nchi badala ya kujikita katika mambo yenye tija zaidi kwa jamii kama ujenzi wa madarasa, ununuzi wa madawati, uchimbaji wa visima vya maji huko vijijini na miradi mingine ya kimaendeleo?

❷ Inabidi niseme hapa kwamba sasa hali hii imebadilika na makampuni mengi, japo bado yamemakinikia shughuli za burudani ili kujitangaza zaidi, yamejibidiisha sana kudhamini shughuli za kimaendeleo pia.

❸ Makampuni mengi sana yamekuwa yakijenga madarasa na ofisi za walimu, kununua madawati, kuchimba visima, kusaidia vituo vya kulea watoto yatima na miradi mingineyo. Hili ni jambo njema kwani kama tukishupalia tu mashindano ya urembo na burudani basi ni wazi kuwa hatutafika popote.

❹ Ni katika mtazamo huu, ambapo nimefurahishwa sana na taarifa kuwa kampuni moja mashuhuri imetoa shilingi milioni 12 ili kudhamini mashindano ya ngoma za Kisukuma kule Mwanza. Hili ni jambo la umuhimu, si kwa sababu mimi ni Msukuma, bali kutokana na ukweli kwamba wengi wetu sasa tumefunikwa na kungu la utandawazi na usasa kiasi kwamba hatujali tena utamaduni na lugha zetu za mama zilizotulea na kutukuza.

❺ Shughuli hizi za kitamaduni zikiendelea kuimarishwa na makampuni binafsi kama tunavyoshuhudia katika mashindano ya urembo, zitasaidia japo kutukumbusha kuwa sisi ni watu wenye utamaduni wetu wenyewe na kwamba kabla ujio wa watawala wetu kutoka huko walikotoka, tulikuwa watu huru kifikira, kisaikolojia na kitamaduni.

❻ Hongera kampuni hii mashuhuri na Mkurugenzi wenu wa Masoko kwa hatua yenu hii ya kimapinduzi kufadhili shughuli hizi za kitamaduni. Bila shaka makampuni mengine yataiga mfano wenu. Nina hakika tukifanya hivi tutapata kuonja maendeleo ya kutosha.

Imetoholewa kutoka, http://matondo.blogspot.com (2012)

www.xtrapapers.com



**Kifungu D**

# Msichana Aliyetoweka Kwa Sababu Ya Mahaba

❶ Baada ya Pili kuvuta hatua mbili tatu kuvuka mlango wa darasa lake lililoelekeana na ofisi ya Msarifu, alirudiwa na kumbukumbu ya kuwa kesho yake jioni ndiyo ilikuwa nafasi yake ya mwisho kwa kipindi hicho kuiona sura ya chuo cha Tabora muhula huo.
"Nakumbuka nilimtumia mpenzi wangu Moddy barua ikimfahamisha kuwasili kwangu hapo Musoma", Pili aliyatamka kimoyomoyo.

❷ Pindi Pili alipomaliza kujifungulia baraza la binafsi alirejea bwenini akaanza kusafisha karibu kila kilichomhusu katika safari yake. Muhula wa mchana akapiga pasi nguo zake na kuzipanga barabara ndani ya sanduku lake. Jioni hiyo Pili aliporejea kutoka mjini kuagana na baadhi ya rafiki zake mbalimbali aliufikia uwanja wa chuo akajifungulia kumbukumbu tele.

❸ Uwanja wa chuo uliozoea kuwaweka wanafunzi wengi huku na huko, siku hiyo ulionekana mweupe kasoro Pili ambaye alikuwa amesimama kando ya maktaba akifikiria jinsi atakavyoyatambua maisha ya Musoma; maisha ya mji mdogo uliofanikiwa starehe za pekee ukilinganishwa na miji mingine iliyovuma miaka nenda miaka rudi. Mwili mzima wa Pili ulisisimka na kuchemka kila alivyouvuta akilini mwake mji wa Musoma kwa jumla.

❹ Bila ya kujifahamu, Pili aliiutulizia macho ya udadisi maktaba, baadaye akatoa sauti nzito, "unh". Papo hapo akaongoza ujia uliokuwa unaelekea bwenini. Chumbani mwa Pili alikwishapabadilisha muundo wake wa nyuma. Mapambo yaliyokuwa ukutani alikwishayabandua. Picha ya mpenzi wake Moddy ambayo ilikuwa ikionekana kila alipokuwa akifungua kabati lake, alikwishaibandua na kuibana sawasawa ndani ya mkoba wake wa hali ya juu.

❺ Pili akakamilisha maandalizi yake ya safari yake, akatulia kunako kitanda hali akipanga na kupangua mahali atakapofikia huko Musoma. Utashi wa moyo wakati mwingine ulihitaji afikie kwa shangazi wake na mvutano wa mahaba vilevile ulipigania nafasi katika kupata haki yake. Fikira zake zilijaribu kuvuruga ushindani huo kichwani mwake na kila alipojaribu kuvumbua wazo jingine, lilifutika haraka na kurejesha usumbufu wa awali. Mawingu ya mvua huweza kufukuzwa kwa upepo mkali lakini kwa upande wa Pili hapakuwa na kitu ambacho kingeliweza kubadili au kumpatia uamuzi wa mkato.

www.xtrapapers.com



❻ “Nitakata shauri pindi nifikapo huko mbele”, Pili alitoa jawabu huku akiinua sanduku lake tayari kukivuka kizingiti cha mlango. Naye akaendelea kuhesabu hatua kuelekea kwenye kituo cha magari, alimkuta dada yake Justina amefika mbele kutoka chuoni.

❼ Uchochoro alioufuata Pili ulikwishaingia giza na ilimbidi auache na kufuata mtaa uliojaa nuru ya taa. Alipowasili kwenye kituo cha gari, alimkuta dadake Justina pale muda mfupi akiwa na wanafunzi wenzake ambao wengi wao walikuwa wanaelekea Morogoro kupitia njia panda ya Dodoma.

❽ Justina alipokuwa hapo kituoni mawazo yalikuwa hayamweki pamoja kutokana na hamu ya kuwaona wazazi wake kwa sababu kipindi kilichopita alikikilikizia kwa shangazi wake. Hakika maelezo yote yalikuwa sawa.

❾ Magharibi hiyo, chombo kilifika kituoni halafu dereva akaweka kizuio kuwapa abiria nafasi ya kupanda na kushuka. Pili hakuchelewa kupanda ndani ya gari moshi tayari kuelekea Musoma. Safari ilikuwa tulivu; abiria hawakusongamana au kukosa nafasi. Kwa kweli nafasi hii ilimpa Pili wasaa wa kutosha kumudu kufunua picha kamili juu ya shangazi wake, na hususan mpenzi wake aliyetarajia kukutana naye baada ya wakati mrefu kupita pasipo kuonana.

PC Geranija na AS Muwanga, *Doa la Mauti* (1976)

www.xtrapapers.com



**Kifungu E**

# Ati, Mila Hii Ni Unyanyasaji Wa Kijinsia? Wanawake Mnasemaje?

❶ Katika makabila mengi ya Kiafrika, wanawake kupiga magoti wanapowasalimia wanaume au watu wanaowazidi kwa umri ni jambo la kawaida. Upigaji huu wa magoti hutofautiana kutoka kabila moja hadi jingine. Kwa Wasukuma kwa mfano, mwanamke alitegemewa kupiga magoti mpaka chini kabisa hasa anaposalimiana na wazee; na upigaji huu wa magoti ulikuwa bado ni ishara mojawapo ya kuonyesha kwamba binti amelelewa vyema na ana sifa za kuolewa!

❷ Wazo la upigaji magoti limezua maswali kuhusu mila hii kongwe. Je, ni heshima au udhalilishaji? Inabidi tukumbuke pia wanaopigiwa magoti si wanaume pekee bali, mwanamke anaweza kumpigia mwanamke mwenzake anayemzidi umri au anayetaka kumwonyesha kwamba anamheshimu. Na katika jamii nyingine wavulana na hata wanaume ndio hupiga magoti.

❸ Nakumbuka wakati nikisoma katika shule ya sekondari ya Kahororo kule Bukoba, vijana wa Kihaya ndio walikuwa wakipiga magoti walipokuwa wakiwapa watu wazima vitu na jambo hili lilitugutusha sana sisi "Banyamahanga" wa kutoka mikoa ya Shinyanga na Mara.



❹ Kuna njia nyingi za kuonyesha heshima kwa watu wazima au watu wenye mamlaka katika jamii mbalimbali duniani. Lakini mimi nadhani kinachohitajika ni maelewano na utangamano wa kitamaduni. Kwa wakati huu wa dot.com, wakati wa usasa na utandawazi ni rahisi sana kutupilia mbali mila zetu kwa kudai kwamba zimepitwa na wakati. Na wakati mwingine tunaweza kushangaa baadaye tunapokuja kugundua kwamba hata hao "wakubwa wetu" tunaojaribu kuwaiga kumbe hata nao wana mila zinazofanana na zetu tunazojaribu kuzitupilia mbali.

❺ Ninachojaribu kusema hapa ni kwamba ni lazima tuwe waangalifu kwani si kila **[ – X – ]** yetu ni mbaya na si kila mila ya kimagharibi ni nzuri! Mila ikionekana ni **[ – 49 – ]** basi ni lazima tutupilie mbali na kama ni nzuri, ni lazima tuishikilie. Vinginevyo tutapoteza utambulisho wetu na kuwa watu **[ – 50 – ]** na chao hapa duniani! Ni dhahiri shahiri kuwa hakuna kitu kibaya sana duniani kushinda mtu asiye na **[ – 51 – ]** wake. Najua si **[ – 52 – ]** kukosa watu kama hao katika jamii yetu.

❻ Na kama kupiga magoti kwa nia ya kuonyesha heshima ni unyanyasaji, basi inatubidi tutafute njia nyingine ya kuonyesha heshima. Na kwa jambo hili la kupiga magoti, ningeomba hasa wanawake watupe maoni yao. Wanajisikiaje wanapofanya hivyo? Ni kweli wanahisi kuwa wananyanyaswa?

http://matondo.blogspot.com (2010)